# KISIMA CHA MKATA

**SAMWEL OLUOCH**

# KISIMA CHA MKATA

HAKIMILIKI ©2021 NA **SAMWEL OLUOCH**

Haki zote zimehifadhiwa. Nimarufuku na hatia kwa wenye silica za kugushi, kuiga, kubadili, kuchapisha, kutafsiri, kuigiza au kutumia mbinu zozote bila idhini ya mwandishi kupitia kwa wakili kulingana na (*Copyright, Design and Patents Act)* ya 1988.

Mtu yeyote atakayefanya kitendo chochote kinyume na sheria anaweza kushtakiwa.

**ISBN: 9798720410773**

**Kimechapishwa kwa Mara ya kwanza 2021**

**Elong'o Publishers.**
Baruapepe:info@elongopublishers.co.ke
**Simutamba**: +254742433826

**Samwel Oluoch**
**Simutamba: +254725658935.**.
Baruapepe: sautiyamtafiti@gmail.com

**Mhariri**: KakaFred.
**Simutamba**: +254716349065

# UTANGULIZI.

Kisima cha mkata ni riwaya inayozungumzia matatizo ambayo huwakumba maskini. Je , maskini hukumbana na majanga yepi? Utapata visa vitakavyokuacha kwenye chumba cha sononeka. Mwandishi amechora picha halisi inayotokea katika maisha yetu. Maskini hupitia mambo mengi sana mathalani: unyanyasaji, dhuluma za haki, ukatili na hata mauko.

Malengo yamesawiriwa vilivyo ili kumpa msomi yeyote mbinu chanya ya kukabili maisha. Asilimia kubwa ya waja hukata tamaa pasi na kujua kuwa baada ya giza ni nuru. Nusra mwandishi akate tamaa lakini kwa msaada wa mwandani wake hakufanya hivyo. Nilikitunga kwa ajili ya kukuza lugha ya Kiswahili inayotumika sana katika nchi ya Kenya, Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi, Afrika ya Kati, Afrika Kusini na kwingineko duniani.

Utawapata wahusika wawili wanaohangaishwa nankunyanyaswa si kimapenzi si kifukara nk. Je kipi kikichosabisha wao kujikuta katika hali hiyo? Pata ufahamu kwenye kisa hiki.

Pata utamu wa matumizi mbalimbali ya tamathali za lugha kulingana na kiwango kilichokusudiwa.

Wa'Salaam!

**Samwel Oluoch**

Jua lilitua kitepetevu kwenye janibu za magharibi. Miale yake ilijaa na kukolea mabaka meusi tamthili ya kaniki. Ingawa sikuwa mnajimu wala mshirikina ishara hizo zilifumbata kitendawili Fulani. Taswira hizo zilizua mjadala moyoni mwangu. Ilikuwa imepita miezi miwili tangu nilipotoka shuleni. Singeweza **kuuma meno** katika hali ile tena. Ama kweli ishara ya magumu ni dalili ya mema yenye mkoba uliojaa mema. Kuvumilia kwangu kulizaa matunda. Naam, matunda yenye Machungu kama shubiri. Kuyaonja yakawa sawa na kutia kaa la moto ulimini. Yalikuwa machungu kiasi cha kwamba hata mbuzi na wanyama kama vile ngamia walao majani machungu zaidi duniani wasingeweza si tu kuonja bali pia kunusia.

Nilivumilia na kuvumilia labda ndiyo iliyokuwa zamu yangu kutokana na ratiba ya **Qurdusi**. Matarajio kemkemu yalinitawala kuwa ipo siku hali ingebadilika. Nilisubiri nikasubiri kwa hamu na ghamu nile mbivu lakini wapi. Si walisema mvumilivu hula mbivu? Huenda yangu ilikuwa changa. Mbivu ikaadimika tamthili ya kaburi la baniani. Ni lini dau la mnyonge likaenda joshi kama si Mungu kupenda? Ni lini kuku wa **mkata** alikataga na kuangua mayai yake salama salmini? Yakawa matumaini ya kumwona ng’ombe wa mkata akizaa pacha.

Licha ya yote, nilikuwa nimekata kauli. Ulikuwa uamuzi uliochemsha damu ya mlezi wangu, Bi. Hamasa. Ulikuwa uamuzi uliotishia kunizamisha katika kaburi la ahera kama alivyodai mlezi wangu. Ulikuwa uamuzi wa kumtenga. Kwake alijua tungetengana kama mbingu na ardhi. Kwangu nilikuwa na

uhakika kwamba ningerudi kwake na kwenye kijiji kizima kuwabainishia kuwa aingiaye msituni hutoka na kuni na aendaye machinjoni hakosi tone la damu. Niliamua kuenda mijini kusaka ajira.

Bi. Hamasa alipokezwa talaka ya lazima na bwana wake. Alitalikiwa miaka minane iliyopita. Talaka hiyo ililazimishwa na ajali isiyojali. Isiyo na kinga wala kafara. Wakati huo nilikuwa katika darasa la nane. Kama desturi ya nchi yangu nilipaswa kuufanya mtihani wa kitaifa. Ulikuwa mtihani ambao ungenivusha katika shule ya upili. Kabla ya kuaga kwake alinishauri kutokata tamaa aushini. Niwaige **wandani** wenye mienendo bulibuli wala si benibeni. Nami nikakua katika msingi huo: wa bidii heshima na utumwa wa mashauri ya wakuu wangu. Sikujaaliwa kuwa wembe masomoni. Nilikuwa kisu butu ambacho daima kilitegemea tupa ya walezi. Walezi wangu walininoa si kanisani si shuleni si nyumbani. Nami nikanoleka. Kweli, kinolewacho hupata.

Sikuwa na tamaa dhidi ya mafanikio ya wenzangu waliokuwa moto wa kuotewa mbali. Sikutaka kuulalia mlango wazi **sudi** ya mwenzangu. Nikakumbuka usemi uliokita mashina na kushamiri vinywani mwa wakale, tamaa mbele mauti nyuma? Nilijikuna nilipojipata. Miaka nenda miaka rudi, nilipita darasa moja hadi jingine. Sikujipata miongoni mwa wale ambao iliwabidi wavyele wao kuja shuleni kushauriana na walimu ndiposa waingia katika darasa jingine. Heshima na intidhamu vilifaa na kunivaa.

Mlezi wangu, Hamasa alikuwa maskini wa mali. Hata hivyo Mola alimtunuku utajiri mkubwa wa nasaha. Katika masuala hayo nisingeweza kumtofautisha na marehemu baba yangu. Maneno yake ya mwisho nilipoamua kuenda kutafuta ajira mjini yangali moyoni mwangu. “Mwanangu umeondoka. Unaenda mjini. Tafadhali yakumbuke yafuatatyo: usije hata kwa siku moja ukamsahau rafiki wa dhati, wazazi ukoo na kanisa. Naomba uende kwa hisani na upatapo ya kheri nilipie ya hisani. Kumbuka akili isalie mjini ila maendeleo yateme kijijini. Epuka makundi hasi yanayopenda vya kisasi. Anasa ni sumu itakayokunasa kwa asasi ya upotovu. Umeenda kwa basi sitaki urejee kwenye jeneza. Nakusihi sana ule na mungwana usile na mgongaji. Safari njema. Wewe ndiwe daraja la kutuvusha kutoka kwenye bahari ya **uhawinde** lama kisiwa cha ukwasi.”

Niliyatega masikio ndi huku kauli zake zikijipenyeza hadi kwenye kilindi cha moyo wangu. Nasaha hizo zilinikuza hatua baada ya hatua. Kama si nasaha zake nisingekuwa mtu mwenye utu bali kutu. Labda singeitwa mtu maana mtu ni utu. Baada ya abu yangu kugura kutoka sayari ya tatu, maisha yalichukua mkondo mwingine. Juhudi za mama kunilipia karo ziliambulia patupu. Ili kufanya mtihani wa kitaifa sharti mja angetozwa shilingi mia nne. Kama hamsini ya kununua mboga na viungo ilikuwa wali wa daku seuze mia nne za usajili. “Mwanangu usijali,” mama aliniambia kwa huruma. Baba yake Yohana ami yako aliniahidi kuwa angekulipia karo ya shule.” Maua ya matumaini yalianza kuchanua tena mtimani.

Jioni moja baba Yohana aliingia kwetu akiwa kwenye shangingi lake la kifahari. Alinijuza kuwa nisahau ziaravya mjini kwani angenipeleka skulini na kunilipia karo yote. Moyo wangu ulijawa na furaha kama mithili ya mvuvi aliyekinasa kishazi cha samaki. Nilijua fika kuwa ningeenda shuleni siku iliyofuata. Siku ya siku ilipofika nilienda shuleni nikiwa na furaha riboribo. Ndoto yangu ya kuwa wakili ilionekana kwa umbali. Nikaanza kujikaza kisabuni masomoni. Ungeniona ungedhani nilikuwa mchwa anayejenga **kishirazi** kwa mate. Nilizamia matopa nikiyabukua ili niweze kubobea na kutopea katika nafasi za Maisha.

Nilikuwa mfano wa wakili atafutaye neno la ushahidi kwenye mashtaka. Baada ya mwezi mmoja shuleni masomo yalikuwa yameshika kasi. Nilikuwa nimesajiliwa katika darasa la nane. Asubuhi moja kengele iligongwa. Sote tulitwika maguu begani lama gwarideni na kusimama huko tisti kama chuma cha pua, tupilia mbali askari gwarideni.  Mwalimu mkuu alionekana mwenye huzuni. Uso aliukunja. Makunyanzi yakamtawala wajihini. Bashasha yake ya kawaida iliyeyuka kama umande wa alfajiri jua linapochomoza. Mkononi mwake alikibeba kijikaratasi. Baada ya dakika chache za kushauriana na naibu wake. Alianza.

“Naibu wa mwalimu mkuu Bw. Leparan, mwalimu mwandamizi Bi. Chelang’at,  mwalimu wa zamu Bw. Milton, walimu, viranja wa shule yetu ya Imara Daima na wanafunzi wote hamjambo? Nina furaha na raha kukithiri ya **buda** aliyeota buri. Kisa na maana, ni siku nyingine njema ambayo

tumetunukiwa na Mwenyezi Mungu Subhana wa Taala. Nina uhakika kama mauti kwamba hakuna yeyote aliye na mwao wa gwaride hili la dharura.

Ukiona mfalme ameitisha kikao katika siku ya Sabato jua kuna la dharura aidha mbiu ya mgombo ikilia kuna jambo. Ninawasheheneza shukrani sufufu kwa kufika na kuwasili yakini, chelewachelewa utampata mwana si wako. Kweli mtu hakatai mwito bali aitiwalo. Lengo la gwaride hili ni kuwakumbusha kuwa malimbikizi ya karo yanazuia shughuli adhimu za kila siku za shule. Wengi wenu mna madeni makubwa sana. Ukweli halisi ni kuwa madeni haya yanaweza hata kuinunulia shule hii ndege si gari. Hivi sasa nachukua nafasi hii kuwatuma nyumbani ili mkalete karo ya shule. Iwapo utaitwa utajongea upande wangu wa kulia. Nyinyi ndio mliokamilisha karo ya shule.

Sanare Mkwasi, Cammilla Lodi, Pilaso Tajiri, Lemashon Pesa, Leshan Ndarama, ………" Majina yalisomwa moja baada ya jingine. Nilikuwa na uhakika kuwa langu lingesomwa wakati wowote. **Ami** yangu aliniahidi kunilipia karo baada ya baba yangu kulala usingizi usio na macheo. Sikuwa na wasiwasi wa mwasi kwa kuwa ami alifuga mifugo wa pesa. Si kitini si mezani **fulusi** zilitapakaa na kukita mizizi kotekote sebuleni mwake.

Mende na viroboto wote kijijini walihamia kwake wakidai sisi tulikuwa mikono mitupu isiyorambwa. Mwalimu mkuu bwana Nchoe Wazi aliendelea kutamka yale majina.

“Dennis Njenje, Evans Dirhamu, Ronald Hela,” Jina langu halikuwa limetajwa. Chembechembe za **hawafu** zilianza kutitirirka tiriri akilini mwangu. Akili zangu mshamara zilinizungusha kama mpira ugani. “Huenda jina langu lilikuwa limesahaulika.” “Hatimaye anayetukamilishia majina ya waliokamilisha karo ni ……. Ko ko ko ko ko.” Ghafla alianza kukohoa. Jambo hili lilizidisha hamu iliyojaa kwenye mioyo ya wengi. “Kunradhi wa mwisho katika orodha hii ni Nkoitoi Fedha.” Maskini Mungu wangu. Sikutajwa. Nilitamani kulia nikajikuta natabasamu. Nilipanga kuanza safari ya kuenda nyumbani shingo upande. “Ami ametuteka bakunja?” Nilijiuliza.

“Nyinyi mliosalia kimbieni nyumbani harakaharaka mkawajuze wavyele wenu kuwa karo yatakikana. Yeyote asithubutu kurejea shuleni bila asilimia sabini ya masalio. Isitoshe, usimruhusu mzazi wako kukuambia uje shuleni eti atatafuta. Bila shaka usikubali kuja shuleni eti mzazi anesema anakufuata. Tafadhali andamana naye kama siafu waendao kuhemera. Nendeni mastakimuni moja kwa moja. Msiwe mbwamwitu kurandaranda hapa na pale mjini. Basi la shule litawabeba kutoka humu shuleni hadi barabarani mtakapoabiri magari mbalimbali ya kuwapeleka manzilini kwenu.

Kunaye anayedai kwamba hajatajwa ilhal alilipa karo alilipa? Vilevile kunaye anayedai kwamba ametajwa ilhali hakuwa amekamilisha karo yake?” Nilitamani kunyosha mkono wangu ila **hisimseto** zilinikinza. Mwalimu mkuu alikuwa mja aliyekuwa na kiwanda cha kutengeneza matusi na karakana ya

kukarabati kamusi za cheche za **subu**. Kila mara aliwakemea, kuwafokea na kuwatweza wanafunzi ambao walijipata katika 'upande mwingine.' Nilitamauka. Kwa kuwa nilikuwa na uhakika na ufadhili wangu nilikata kauli kuulizia kiwango cha deni langu.

"Wewe Maskini mwana wa Hamasa, tangu lini ukalipa ama hata kulipiwa senti yoyote humu shuleni. Wewe ni baadhi ya wanafunzi walao vya wengine na kujaza misala ya humu shuleni. Wewe ni zaidi ya kupe. Mara ya mwisho sarafu chache kulipwa ilikuwa miezi miwili kabla ya baba yako kwenda jongomeo". Habari hizo za msiba zilinipiga mshipa na **kunigoga** roho. Macho yalinitoka pima kinywa kikabaki wazi kama spana pango la popo kando. Nilipigwa na butwaa chakari nisijue wa kumlaumu. Nilifikiria kumlaumu mwalimu wangu. Alikuwa tajiri wa kutajwa na kutajika si mashariki si magharibi. Nilimtarajia anipige jeki. Anitilie pondo. Dua langu likawa sawa na la kuku lisilompata mwewe.

Mara nikaona kwamba nimlaumu mama yangu. Kwa nini alikubali kuwa mkata. Umaskini ulimwandama na kumvamia kama vile nzige walivyovamia mashamba ya wakenye kipindi kilekile ukongo wa Uviko-19 ulipobisha nchini humo. Daima alijisetiri kwa mademu na vitema. Hatimaye nilimlaumu baba yangu mzazi kwa kukubali kufarakana na sayari hii ya tatu na kurudi kwa Baba ni lilahi ina ilahi rajiuna. Kweli Maisha ni mshumaa, unapozidi kuangaza ndivyo

unavyozidi kuyeyuka na kumalizika. Maisha ni ukungu, lichomozapo jua la mauti hayana budi kutoweka. Maisha huisha.

“Mara tatu mfululizo nikiwatuma wanafunzi karo huwa nakuhurusu darasani. Sasa hivi huna budi kuenda nyumbani.” Machozi ya majonzi yalinitiririka kama mifereji ya maji yatokayo kwenye **bilula**. Yaliniloa rovurovu nikawa sawa na mkunga baharini. Kwa kweli nilifikiria kuwa nilikuwa nimelipiwa karo kwa mwezi mzima kumbe nilikuwa nikifarijika kwa huruma ya mwalimu huyu. Hata hivyo ni lazima atangaze hayo hadharani? Nilijiuliza. Sina baba. Mama naye nilihofia maisha yake. Kumpata akiwa salama salmini kulikuwa ni kubahatisha. Kwake maisha yalikosa maana na yakawa sawa na kaka tupu la yai. Chakula kiliadimika kama barafu ya kukaanga. Kwake heri mate tumboni akawa anategemea maponeo.

Niliogopa kufia nyumbani. Sikutaka nimwone mama yangu alivyokuwa. Kumwona kungeniliza siku zote za kuishi kwangu. Sikutaka kuyaona macho yake yaliyojaa huzuni na majonzi. Sikutaka kuyaona mavazi yake mararumararu yaliyochanika si mithili ya kondoo aliyeugua. Sikutaka kuziona nywele zake zilizofanana na **dhikiri** ya nzi. Zenyewe zilimtimka timtim kama kondoo mwenye manyoya haba. Sikutaka kuviona viatu vyake vilivyokuwa vikiicheka hali yake. Sikutaka kuiona miguu yake ya mvungu. Sikutaka kuyaona macho yake yaliyojaa na kujazana makunyanzi na makunyato. Sikutaka. Daima sikutaka. Hata hivyo. Ng’ombe akivunjika mguu malishoni

hujikokota hadi zizini. Nilizama kwenye lindi la mawazo. Mashua ya mawazo ilinisafirisha kutoka hali hii hadi ile.

Safari ya kuenda nyumbani ilianza saa moja macheo. Basi lilikuwa limeshiba kwa wanafunzi waliokuwa na mseto wa mawazo. Wengine walifurahi mno. Naam, kundi hili lililifanya basi kujaa shangwe, nderemo, vigelegele, vifijo, chereko na kayaya za ndani kwa ndani. Wa kupiga **siwa** walipiga. Wa kupiga mbinja walipiga. Wa kupiga makonzi walipiga. Lengo likawa kuwasili nyumbani na kuonana ana kwa ana na wapendwa wao na pia kupata fursa na satua murua ya kufanya watakalo pasi na sheria za skuli kuwazuia.

Mitibwiriko na bahwabahwa zilipamba moto na kushika usukani. Vicheko na tabasamu viliundika kotekote. Hawakukosekana waliokuwa kwenye kinamasi cha majonzi. Nilikuwa mwakilishi wao. Garini tulikuwa wachache sana. Kundi hili lilipukutikwa na machozi ya majonzi kupukupu. Wengi wa hawa walibanwa na kiwewe kisicho na kipimo wala mizani. Kwangu hofu iliniteka nyara. Nikapumbaa na kukosa la kufanya. Dunia nzima ikaniyumbisha na kunizungusha kama tiara. Nikawa napiga mbizi katika nchi kavu. Nilijutia nafsi yangu. Nilijutia wazazi wangu. Nilijutia Maisha yangu. Nilijutia majirani zangu. Nilijutia kila mmoja aliyezaliwa katika sayari hii ya tatu. Nilijutia kuzaliwa. Nilibaki nikiwaza na kuwazua mithili ya mja anayeishi maisha ambayo asilani si yake. Hatimaye nilifika nyumbani. Hakukuwa na yeyote. Nilitulia chini ya mti kumsubiri mama kufungua mlango wa nyumba yetu ya msonge iliyojiinamia kwa masikitiko. Nilichukua muda mrefu pale.

“Maskini amka,” sauti ya mwandani wangu Hadaa ilinizindua. Nilikuwa chini ya mwembe uani. Usingizi ulikuwa umenishona nisijifahamu wala kujijua. **Sikumaizi** kuwa katika muda huo wote nilikuwa nimezama kwenye ndoto. Hadaa aliponigutusha, nilikurupuka ghafla kama Sungura aliyemwona kelbu. Nilijilaumu kwa kuamka kwa sababu kuamka kwangu kulinikumbusha mengi ….. ninakoelekea.

“Naam Hadaa sema?” Niliamua kumsikiliza sahibu wangu.

Machozi yalimlengalenga mwanzoni. Kufumba na kufumbua yakaanza kumtiririka tiriri. Hatimaye yakawa yanampukutika kupukupu. Yakamloa akawa mfano wa **chuchunge** kwenye ziwa Viktoria. Alinitonesha machozi. Hakuijibubsalamu yangu. Akanikumbusha hali yangu. Nilivyozidi kuililia hali yangu ndivyo naye alivyozidi kuililia hali yake. Hakukuwa na wa kumfariji mwenzake. Likawa swali la kilio linajibiwa na kilio. Kila mmoja wetu alikuwa na mwao kuwa mmoja alikuwa akimwonea mwenzake **mbawazi**. Kumbe kila mmoja alikuwa akipambana na hali yake. Ilibidi kila mmoja ajifariji baada ya dakika thelathini hivi. Baadaye alianza kunihoji.

“Lipi linakuliza?” Nilikosa jibu. Kisa na maana nilikuwa na uhakika kuwa kwa kurejelea yaliyotokea gwarideni kila mtu aliifahamu hali yangu.

“Mwenye macho haambiwi tazama,” niliamua kumjibu.

“Dada yangu nami sina pa kuenda. Afadhali wewe una mlezi Bi Hamasa nyumbani. Ni hadithi ndefu lakini naomba nikusimulie kwa muhktasari.

Ulikuwa mwaka jana tukiwa katika darasa la saba. Hapo ndipo masaibu yalipobisha mlangoni petu. Bila kuchelea nikaufungua mlango. Ikawa kwamba mgeni njoo mwenyeji apone. Mgeni wangu wa heshima alikuwa mwalimu mkuu. Huyo aliyekuaibisha gwarideni. Aliyafanya maisha yangu kule shuleni kuwa ya asali na maziwa. Alinipenda nami nikapendeka. Alinilea mle kwa tunu na tamasha. Pale nikapoteza jina langu la Hadaa akaanza kuniita sabuni yake ya roho. Kila aliponiita ofisini mwake kinywa chake kilitamka, *“I love you my sweet heart. You are the most beautiful girl in Bidii school. The only fish in Lake Victoria*. Uzuri wako utakufaa. Utakulipia karo. Utakununulia sare. Utakupeleka ziara bila malipo. Utakupa uongozi humu shuleni. Utakuongeza alama bila kutokwa na hata tone la jasho. Utakutembeza kwangu. Utanifanya nikuone nawe utaniona.”

"Mwalimu mkuu? Huyu mmoja! Potelea mbali! Ndiyo hulka yake. Dada maneno matamu humtoa nyoka pangoni. Heri nyinyi wenye urembo!” Nilimkatiza usemi.

"Miguu yangu ilitii amri ya kumtembelea kila wikendi. Macho yangu yakawa hayaoni chochote ila yeye. Nyakati zote. Si wa Kiswahili si wa Kiingereza. Funzo la Hisabati nalo sikuambii. Mara alipoingia darasani mwili ulinisisimka. Alama nazipata hata nikilifanya swali kwa lugha ya Kilatini ambayo

hakuelewa kuwa ni miongoni mwa lugha duniani. Tindi moja tindi mbili tindi tatu mazoea. Mimi na mwalimu tukawa chanda na pete. Likizoni na wikendi tukawa kupe na mkia wa ng'ombe. Kumbuka usemi kuwa ukimwona zinduna ambari i papo.

Uhusuano huu ulikolea hadi wakati nilikisa budi kulipa deni. Madeni yalikuwa mengi. Kweli yanazidi yaya haya tunayoendea nyumbani. Si viatu vyeupe kama pamba, si rinda jeusi kama kaniki. Si kuongoza darasani si masurufu za sidiria na malapa ghali. Si kalamu aina ya '*ballpen*' si vitabu vya '*hard cover.*' Kulipa deni kulikuwa rahisi kama kuunga moja na moja ukapate mbili. Nikakubali kwa **hiari** kulilipa. Mchovya asali hachovyi mara moja. Deni nililipa si jioni si alfajiri si wikendi si usiku. Wengine wakidurusu darasani mimi nilikuwa kwake. Wenzangu walijua kwamba nilikuwa nimepelekwa hospitalini. Dada yangu, mwalimu huyo alinigeuza nikawa mke wa tatu. Wajua wawili wa kwanza?" Mshangao ulinikata ulimi nikakosa kusema lolote. Baada ya dakika tatu nikamjibu.

"Namtambua wa kwanza aliyeaga dunia kwa ukongo wa ukimwi."

"Mchezo huu wa bahati nasibu uliendelea kwa muda mrefu. Sikuhofia uhimili wala ukimwi kwa kuwa alikuwa ameniahidi kuwa alikuwa mwenye afya na angekinga ujauzito kwa vyovyote vile. Siku ya kufunga shule umati ulijaa sana shuleni. Aliniarifu niwaite wavyele wangu. Nao kwa heshima na taadhima waliwasili. Wakati huo nilikuwa nambari ya kwanza kabisa kutoka nyuma. Hakuna aliyenishinda kutoka huko.

Tofauti na ile ya saba au tano niliyozoea. Sikuwa nimeyaona matokeo yangu.

Mwalimu wa darasa alipotupa vijikaratasi vyetu vya majibu vyangu aliniarifu kuwa mwalimu mkuu anavipitia. Matokeo yalikuwa yanapewa wazazi moja kwa moja bila mwanafunzi kuona. Hii ilikuwa mbinu ya kuwazima wanafunzi wenye tabia ya kubadilisha matokeo au kuwateka bakunja wavyele wao. Mwalimu mkuu aliniambia kuwa matokeo yangu yalikuwa na kasoro fulani lakini wapi? Mzazi alikuwa ashakabidhiwa. Lo! Ujanja wa nyani huishia jangwani. Kuwapa wazazi bila kupitia kwa mwalimu mkuu kulikuwa njia ya mwalimu wa darasa kutibua njama ya mwalimu mkuu. Wazazi wangu walishawishika kuwa sikufua dafu masomoni.

Njia mwafaka ya kutatua janga hili ni kuhudhuria masomo ya likizoni kwa mwalimu. Wazazi wangegharamika kwa shilingi mia tano kila wiki. Hata hivyo waliahidiwa kutokuwa na **rangaito** kwa kuwa nisingekosa kufundishwa wala kutumwa nyumbani hadi wakakapopata hela hizo. Kupunguza alama kwangu kulitokana na hali kuwa mtihani ulikuwa wa mwigo. Mwalimu wangu alienda kuusimamia mtihani huo katika shule jirani. Mgeni aliyesahihisha kazi zangu aliifanya kazi yake bila huruma wala mapendeleo. Nikapata haki yangu. Kweli mja huvuna alichopanda, ukipanda pantosha utavuna pankwisha.

Wazazi wengi walihitaji masomo hayo za ziada kwa wanao ila mwalimu mkuu alikataa katakata. Aliwajibu kuwa

alikuwa na shughuli **belele** zikiwemo za kifamilia. Pamwe na hayo alikuwa anaendelea na masomo ya juu katika chuo kikuu. Ikawa ishara tosha kwamba asingepata hata sekunde ya kumfaa mwanafunzi yeyote. Nami aliniahidi kuwa angenifaa kwa hali na mali ukipenda kwa jua na mvua. Masomo haya yalipaswa kuendeshwa nyumbani kwa mwalimu mkuu. Serikali hapo awali ilikuwa imepiga marufuku masomo ya likizoni shuleni. Ilikuwa kawaida ya walimu wetu kuwafunza wanafunzi fulani maskanini mwao.

Mimi kuenda kwa mwalimu mkuu kukawa kawaida kama jua kuchomoza na kutua. Kila siku nilikuwa nikienda kwa mwalimu wangu ili aniongoze. Kweli 'aliniongoza.' Mama yangu alimpenda sana mwalimu wangu. Kila asubuhi nilikuwa ninambebea chapati, chai, mandazi maziwa na vingine vingi vya rejareja. Kumbuka mja hujikuna ajipatapo. Kwa mama yangu hizo zilikuwa hedaya kubwa sana kwa 'mwelekezi' wangu. Kila asubuhi nilipofika, mkewe alinibakishia kiamshakinywa. Nilikitendea haki yake kisha masomo yakaanza. Bada ya wiki ya kwanza, mwalimu mkuu alimruhusu mkewe kuenda mashambani kwa likizo. Hapo nikaanza kuyalipa madeni kwa hiari.

Niliporudi nyumbani aghalabu huwa nilikuwa na uchovu mwingi sana. Mara si moja nilikuwa dhaifu mithili ya mkufu. Mwili wangu uliregea regerege kama utumbo wa samaki. Parafujo za mwili wangu ziliregea regerege kiasi cha nzi kunibwaga chini kwa kishindo ikiwa angalitua popote mwilini pangu. Nikawa sina uwezo wala kani hata wa kupesa kope wala

kumeza mate. Siku ambayo sitaizika katika kaburi la sahau ilikuwa Ijumaa fulani. Sikurauka na kujihimu namna ilivyokuwa kawaida yangu. Nilipoamka saa tatu nilishangaa mno. Huo ndio wakati ambao masomo huanza kule kwa mwalimu wangu. Mimi huyo sijakoga wala kusebeha.

Nje kulipambazuka ajabu. Dunia tayari ilikuwa imeanua joho lake jeusi tititi kama kaniki na kulialika jua kushika hatamu. Jua nalo lilitapanya miale yake tukufu katika kila pembe ya sayari yetu. Ndege hawakuwepo tena. Niliwazoea kughani nyimbo zao angani wakikorokocha kwa sauti wazijuazo wao. Niliwazia kuenda hamamuni kushtaki machovu na uchege. Nilikuwa nimenyong'onyea na nikawa sina udole. Uchovu ulinizika na kunitia maumivu makali. Nilijitia nguvu za bandia lakini wapi? Ni nani aliyekwisha kufaulu kuupanda mgomba akavuna viazi?

Nilipofika na kuwasili hamamuni nilijitahidi kwa jino na ukucha kupambana na hali ile. Hakika, mfa maji hukamata maji. Waaidha, mfa maji haachi kutapatapa, nilijipinda mgongo kama upinde na kuyavamia maji yale. Kweli maji ukiyavulia nguo yakoge? Maji baridi shadidi yaliamsha dalili zote za maradhi yote nilikuwa nayo. Si kutapika, si kuzizima, mara joto jingi mara kichwa kuwanga. Nilitamani hata kaka yangu aje bafuni aninusuru. Yote yaliambulia patupu. Mimi Hadaa ndiye niliyekuwa **chudere** katika aila yetu. Siku hiyo mama alikuwa ameenda katika hamsini zake. Baba ndiye aliyekuwa nyumbani.

Je, ningemwita aniauni? Mimi bintiye aliyebaleghe? Wakati huu nilikuwa nimeoga. La kujiosha. Nilijiosha kwa matapiko yaliyokuwa yakinuka kama mzoga wa panya. Niling'ang'ana na kupambana ha hali pale **hamamuni** hadi nilipofua dafu kujimwagia maji na kujivisha. Nikademadema hadi chumbani mwangu. Nikiendelea kujikwatua, sauti ya baba iliniogofya.

"Nimemwona nani? Ni Hadaa binti yangu? Mbona kakonda kama ng'onda? Mbona mchovu. Kwa nini anaonekana anayechungulia kaburi?" Maswali haya yalinikera na kunikereketa maini. Ukingo wa mbio za sakafuni ukaonekana kwa umbali.

Sikutoka chumbani mwangu. Niliyaogopa maswali yale. Ikumbukwe kwamba baba alikuwa amekataa katakata masomo ya likizoni. Alidai kwamba iwapo ni lazima basi mwalimu husika angekuja kunifundishia kwetu akiwa kitini pake akitathmini yanayojiri. Baada ya kukawia pale kwa muda ilimbidi aniite. Nami sikuwa na budi kuitika. Aliniarifu na kunitaarifu nimpelekee maji ya kunywa. Kumbe bwana alitaka kunihoji kwa kuwa alihofia hali yangu. Kumbuka, uchungu wa mwana aujuaye ni mzazi. Nilipomfikia, hakuamini **maninga** yake. Alimwona mja aliyekanwa na mwili wake, afya ikamtoroka na sura kumhepa akawa si yeye.

Uele uliniparamia na kunidhoofisha vilivyo. Ngozi yangu iliparara na kuwa na mabakamabaka sikuambii ya chui. Nilibakia wa leo, kesho. Nikawa ninachungulia kaburi. Mguu

mmoja kitandani mwingine kaburini. Nguvu ziliniisha mwilini nikabaki kvuli. Kwa kuwa chelewa chelewa utampata mwana si wako, baba aliamua kunipeleka hospitalini. Alikuwa hawinde bin chochole. Dau lake liliyumbayumba na kuzama zi katika bahari ya ufukara iliyojaa mawimbi ya matatizo. Hakujali hali yake. Alinibeba mgongoni hadi kwenye zahanati. Ni lini ndovu aliwahi kushindwa kubeba pembe zake?

Mama yangu aliyekuwa akiendelea na kibarua chake cha kufagia hospitali alimaka alipotutupia maozi. Kwa haraka akajongea mahali tulipotua.

"Mume wangu pole sana hali yako imekuwa mbaya zaidi? Alimwuliza huku machozi yakishindania mwanya wowote uliokuwa machoni pake. Alimfahamu mume wake kama mja asiye na ngoma wala maulidi. Mabega yalimwanguka na kumwaika kama kikongwe. Alikuwa ameiabiri meli ya kuenda kaburini. Kuonekana kwake kukawa kunasababishwa na kukawia kwa meli hiyo baharini. Hata hivyo meli hiyo ilionyesha dalili za kufika bandarini. Mama alishangaa nilivyopata habari za baba na kutoka kwa mwalimu wangu kuja kumsaidia. Aliniona kama akiba kubwa sana katika familia yetu. Kumbuka, akiba si mbi ingawa ya kumbi siku ya kivumbi hutia motoni. Baba alimwambia kuwa mimi ndimi mgonjwa wala si yeye. Mama alishangaa kuona kuwa anayechungulia kaburi hunionea huruma. Ikawa kinaya kikubwa sana.

Kwa kusaidiwa na manesi pale hospitalini nilibebwa hobela hobela hadi kwenye **sadaruki**. Mle madaktari

hawakuchelewa. Matibabu yalianza rasmi. Damu ilipimwa mara kadhaa, mkojo haukusazwa. Shinikizo la damu ikafuata. Kiwango cha maji mwilini kikafuata. Mara uyoka, mara sindano, mara stethoskopu mara pimajoto. Kila aina ya mashine yalitumika kwangu. Ilmuradi nipate uhai.

Mama na baba waliitwa mle chumbani baada vipimo kadha wa kadha. Madaktari waliwakagua na kumruhusu mama kutoka ili baba abaki. Baba alionekana mkakamavu na mwenye uwezo wa kustahimili machungu. Hawakujua hali yake kiafya. Nami nilitegea kwa makini sana mazungumzo yao.

'Bwana we umefanya jambo bora sana kuchukua hatua hii mama alipokuwa mbali. Kwa kweli ungechelewa huenda kwa sasa tungekuwa tunazungumzia za tanzia'.

Baba alikipigapiga kichwa chake ishara ya kuridhika na maelezo ya daktari. Dakatari aliendelea. 'Tumevifanya vipimo takribani kumi na viwili.” “Kumi na …….” baba alimaka. “Hakuna kipimo ambacho hakijazaa matunda. Kila kitu na hali tulizoshuku zimegonga ndipo. Baadhi tu ya matokeo muhimu ni haya.” Daktari alimkabidhi karatasi ili baba ayasome matokeo namna alivyoyaandika daktari.

Baba hakuamini masikio yake. Alidhani kuwa yalikuwa yakimchezea shere. Alianza kutetemeka kwa hasira mithili ya **tete** motoni Ukachukua muda mrefu sana atulizwe na wauguzi wale ambao kamwe hawakutaka mama awe na habari. Taarifa hii ya daktari iliamsha magonjwa yote aliyokuwa nayo baba.

Kabla ya kupoteza fahamu mle chumbani alisema kwa ukali. “Mtoto wangu wa pekee umeniaibisha. Nani atayarithi ile nyumba yetu ya msonge. Urithi ni urithi hata kama ni vazi. Hata kama ni meza. Hata kama ni malapa. Hata kama ni sakafu pekee ya nyumba. Hata kama ni unyasi wa paa.

Mwalimu mkuu amenisababishia janga ambalo sikuwahi kufikiria. Atakoma! Atakoma! Ni lazima kama ibada nimkomeshe! Daktari nakuomba uniandikie waraka unaoonyesha namna mwalimu wangu amekuwa akimdhalilishwa kimapenzi mwanangu. Mungu wangu! Mungu wangu! Mbona waniacha? Imekwisha!” Kilichofuata mle chumbani kilikuwa sauti kama ya gogo lililoanguka sakafuni. Baba yangu alipoteza fahamu papohapo na akaaga dunia mara hiyo hiyo. Ningekuwa na uwezo wa kuzungumza na Mungu, ningemsihi amrejeshe baba duniani ili mwenyewe niage dunia. “Mwalimu huyu sharti tumsaidie mama mtoto kumchukulia hatua,” daktari alisema kwa hasira. Sikujua nimtetee mwalimu wangu au nimkane. Kila dakika nilikuwa nikitia na kutoa. Nikifikiria jibu nitakalojibu iwapo ningeulizwa kuliendaje.

Daktari aliinama kitandani pangu na kwa haraka akaiandika barua ile ya uhamisho. Nilipolala nilikuwa nikichungulia kwa makini sana anachoandika. Alikuwa na jukumu la kuziandika barua mbili. Ya kwanza ilikuwa ya uhamisho ya pili ikiwa ya kumshtaki mwalimu wangu. Nakala zangu ninazo hapa.

DAKTARI CHUNGUZA MAMBO,

ZAHANATI YA MAAJABU,
S. L. P. 9874 – 213333,
TAABU.

12/11/2019.

HOSPITALI KUU YA TIBA BORA
S. L. P. 7576- 736447
NAIROBI

Kwa daktari mkuu,
<u>MINT: MATIBABU YA HADAA TAABANI</u>
*Kwa kurejelea magonjwa yaliyotajwa kwenye matokeo ya lebu, zahanati ya Maajabu inakuomba kumfaa Hadaa kwa matibabu thabiti. Zahanati hii haina wataalamu wa kuyatibu magonjwa ya zinaa. Mbali na hayo, kupitia kwa uwezekano wa mgomo wa madaktari na wauguzi nimehisi ni vyema aje kwenye taasisi hiyo ambayo ni ya kibinafsi. Zahanati hii aidha, haina dawa za kupunguza makali ya ukimwi. Isitoshe, hata Panadol ya kutuliza maumivu hatuna. Kumbuka pamoja na masuala mengine kama vile kutolipwa kwa wafanyakazi yamechangia mgomo utakaoshuhudiwa wiki ijayo.*

*Mwele huyu yu katika hali mahututi. Hawezi kupata matibabu kisha arejee nyumbani. Safari hiyo inaweza kukatizwa ghafla na mvua. Naam, mvua y amauti. Ambayo dalili zake ni wazi kama meno ya ngiri. Kwa heshima nakuomba ushughulikie swali hilikama la dharura mno zaidi ya yote mliyo nayo kwa sasa.*

*Ni mimi wako mwaminifu*



*Dkt.Chunguza Mambo*

Baada ya kukamilisha uandishi huo wa kwanza alizama katika barua ya pili. Barua ambayo ilinuia kunitetea. Si mimi tu bali pia mabanati wengine ambao huenda wamepitia au wanapitia hayo niliyoyapitia. Pale pale kitandani alianza kuuandika waraka wa pili. Waraka huu ulipaswa kuwasilishwa kwenye kituo cha polisi ili mwalimu wangu aweze kuchukuliwa hatua. Hebu yapitie aliyoyaandika daktari.

*DAKTARI CHUNGUZA MAMBO,*
*ZAHANATI YA MAAJABU,*
*S. L. P. 9874 – 213333,*
*TAABU.*

*12/11/2019.*

*KITU CHA POLISI CHA WAJIBIKA*
*S. L. P. 3657 – 8765*
*SALAMA*

*Kwa O.C.P.D,*
*YAH: RIPOTI YA MWALIMU KUMLAGHAI NA KUSHIRIKI MAPENZI NA MWANAFUNZI.*
*Haya yalijiri mnamo siku ya Jumatatu mtoto wa umri wa miaka kumi na minne alipofikishwa zahanatini kwa matibabu. Mhusika alionyesha dalili za magonjwa kadha wa kadha ya zinaa yakiwemo: UKIMWI, Kaswende na Kisonono. Kwa kurejelea utafiti wa madaktari, ilibainika kuwa alikuwa na magonjwa hayo hatari. Sasa hivi anachungulia kaburi katika hospitali ya Tiba Bora. Sina uhakika na anavyoendelea ama hata ashaaga dunia kwa kuwa kila aliyemwona alimtakia afueni ambayo tafsiri yake kamili ilikuwa ni kumuaga afike mahali pema peponi.*

*Kulingana na alivyoeleza mwanafunzi, mwalimu mkuu anayefahamika kama Chinja Ua, ameshiriki naye katika tendo*

*hili si mara moja si mara mbili. Tendo hili lilianza kitambo mno tangu alipokuwa katika darasa la saba. Tendo hili lilikolea katika darasa la nane mwaka huu. Mbali na kuambukizwa maradhi hayo matatu, mwalimu huyo alimtia mhasiriwa ujauzito. Pamoja na mwalimu huyo wamekuwa wakiendeleza juhudi za kuavya mimba hiyo. Juhudi hizi zimesababisha kifo cha malaika asiye na doa tumboni mwa mhasiriwa. Hili ndilo jambo ambalo huenda likamsafirisha jongomea wakati wowote kuanzia sasa.*

*Nakuomba kwa heshima na taadhima umchukulie mwalimu huyu hatua ili haki ipatikene. Mwanafunzi huyu hana mtetezi. Baba yake aliaga dunia alipopokea taarifa hizi. Mama yake ni yule mkata ambaye hupata ajaaliwalo si atakalo. Ana deni ya milioni mbili zahanatini humu. Kumbuka sijaongeza gharama ya matibabu ya mwanzo ya msichana wake. Madeni haya yalitokana na matibabu ya marehemu bwana wake. Ameifanyia kazi zahanati hiiilikulipunguza kwa miaka mitano. Hapunguza hata nusu yake. Kwa niaba ya aila hii ya watu wawili kwa sasa naiombea haki kutoka kwako. Nina matumaini si* ***kidigi*** *kuwa hatua Madhubuti za kukomesha unyama huu utachukuliwa. Nitakuwa tayari kuwasilisha ushadi wowote kuhusiana na uchunguzi wa hosptalini. Nakuomba tuungane mikono kukomesha madhila haya. Mwalimu husika ndiye mwalimu mkuu wa shule ya Bidii iliyo kwenye mtaa wa mabanda kule Madongoporomoka. Nambari yake ya simu ni 0725658035. Nambari hizi tulizipata katika simu ya mama ambayo mara*

*nyingi alitumia kuwasiliana na msichana. Ni tayari kwa ushauri wowote ambao utakufaa katika uchunguzi wako. Nambari yangu ya simu ni: 0704687018. Kwaheri.*

*Ni mimi wako mwaminifu,*



*Dkt. Chunguza Mambo..*

Sikujua kuwa mwalimu wangu kwa muda huo wote alikuwa akinihadaa. Isitoshe namna baba yangu mzazi alivyozikwa sina habari. Nilibaki yatima wa kujitakia. Sheria ilipochukua mkondo wake, mimi nilikuwa nimetulia hospitalini sijijui sijitambui. Nilikuwa nikitazamana na **ziraili** aliyekuwa amenikodolea macho yake. Nilitazamana na kifo ana kwa ana. Yaliyotokea kwa sasa nayapata kama hadithi za sungura na ndovu. Kwa Imani natarajia yalikuwa kweli. Niliarifiwa nilipotoka hospitalini kuwa mwalimu mkuu alikuwa ameponea chupuchupu. Alikuwa amekwepa mtego ule uliodhamiria kumnasa na panya. Kumbe alikuwa na habari ambazo sikujua aliyemfahamisha. Alikuwa amempata mama na kumpeleka chemba. Matokeo ya mazungumzo yao yalikuwa ni kwamba mambo yote yaliyotokea yangesuluhishwa nyumbani. Sikuamini kuwa hakimu angekuwa na uamuzi ule. Mama aliahidiwa vitu kochokocho ambavyo sijakiona hata kimoja kikitimia isipokuwa

kusoma. Baadhi ya ahadi zilizomfanya kukosa kuhisi uchungu wa mwana ni kuwa, mwalimu huyo angenioa.

Isitoshe, mwalimu wangu aliahidi kuyadhamini masomo yangu kuanzia darasa la nane hadi chuo kikuu. Mwalimu huyo aliongeza kuwa angemjengea mama yangu jumba la kifahari inasemekana kuwa kulikuwa na ahadi ya kuiondoa aila yangu kutoka kwenye umaskini uliogandamana na kila mtu wa familia yangu. Pamoja na mambo mengine mengi hadi sasa zimekuwa ahadi za uswahilini. Siku moja mama yangu alimtishia kuwa angempeleka kortini tena. Kilichofuata ni watu wasiojulikana kuonekana katika ua wetu kila leo. Watu hawa walimwandama mama yangu kila kulipokucha. Wengi waliwaona alfajiri na hata usiku wa manane. Mara nyingi walikuwa wakivaa mavazi meusi ambayo yalizuia yeyote kuwatambua. Kila mtu alipokutana nao hawakusema lolote. Walijifanya kujipa shughuli. Baada ya mama yangu kuhofia usalama wake aliwaripoti kwa polisi.

Polisi nao walisema kuwa wataanzisha uchunguzi kabambe wa kuwanasa. Duru za kuaminika ziliarifu kuwa yule daktari aliyenifanyia uchunguzi alihamishwa na kupelekwa katika sehemu ya nchi iliyokuwa na ukame zaidi nchini. Alipomudu pale alihamishwa tena na kupewa kandarasi ya kuwatibu wanajeshi ni huko kazini alikutana na kifo chake kambi la wanajeshi lilipovamiwa na magaidi.

Mama yangu alikosa shahidi muhimu sana katika kesi yangu. Hata hivyo hakuenda nguu. Alijikaza kuhakikisha kuwa haki imepatikana. Aliwafikia kila mmoja ambaye angekuwa wa

msaada kwake. Diwani alipofikiwa alidai kuwa ana msururu wa mikutano bungeni hivyo basi mama alipaswa kungoja. Mbunge naye kila mara alikuwa '*busy*.' Juhudi zote za kumpata zilienda arijojo. Hata barua ilipoachwa kuwa akija aisome nikama barua hiyo aliibadilisha kuwa karatasi shashi. Chifu aliyeahidi kumfaa kwa mvua na jua naye hakufaulu. Ilisemekana kuwa mwalimu mkuu alimzungusha mbuyu. Na kumlainisha. Kila siku ikawa mara kuja kesho, mara keshokutwa, mara mtondo mara mtondogoo. Licha ya umaskini mama hakuwa mja wa kutamauka. Aliamua kwamba angemshtaki mwalimu wangu kwa tume ya kuwaajiri walimu nchini. Jambo hilo alinuia kulifanya baada ya siku mbili.

Alipofika aliowapata pale waliahidi kushughulikia jambo hilo. Mwalimu mkuu aliitwa mahakamani kuandikisha kilichojiri. Baada ya taarifa hizo aliendelea na kazi yake ya ualimu. Ghafla niliitwa huko mahakamani kuandikisha ripoti. Sikuchelea nilifanya hivyo. Ilikuwa kazi ngumu sana pale mahakamani. Shughuli hizo kutokana na maswali mengi niliyokuwa nikiulizwa nikachelewa kurudi nyumbani. Jirani yangu mwanafunzi mwenzangu aliporudi nyumbani aliniambia kuwa mwalimu mkuu alisema kuwa wanafunzi wa darasa la nane wangekuwa na mtihani alfajiri siku iliyofuata. Hivyo basi kila mmoja alitakiwa kujihimu ili asije akakosa mtihani huo. Nilimpa habari mama yangu naye akanirausha siku iliyofuata. Nilianza safari ya kuenda shuleni saa kumi na moja alfajiri. Watu wasiojulikana waliniteka nyara. Nilizibwa mdomo nisijua nilipo wala nilpoelekea. Nilikaa kule kwa miezi mitatu.

Niliarifwa kuwa ripoti zilijaa kila mahali kuwa nilikuwa nimeuawa. Kumbe wanafunzi hawakuambiwa wafike shuleni mapema. Ulikuwa mkakati wa mwalimu wangu kusambaratisha kesi iliyotishia kummaliza.

Aidha, alfajiri hiyo ndiyo iliyokuwa ya mwisho kumwona mama yangu. Niliambiwa kuwa alikuwa amepatikana karibu na lango lake akiwa amekufa fofofo. Alikuwa ameuawa kinyama kwa kupigwa na kifaa butu kisogoni. Siku moja nikachukuliwa usiku wa manane na kupelekwa kwetu. Sikuwajua walionifikisha pale. Kulipokucha niliwahadithia majirani kilichotokea. Hadi wa leo dadangu mimi huishi na jirani yangu. Inasemekana kuwa mwalimu wangu alikuwa chanzo cha kifo cha mama yangu na kutekwa nyara kwangu. Huko kwa jirani nimekuwa mtumwa na mtoto wa kambo hadi leo. Angalau wewe unaenda kwenu. Mimi ninaenda kwa jirani aliyejifanya msamaria kumbe ni mbwamwitu aliyevaa ngozi ya kondoo"

Hadaa alikamilisha kisa kilichoniacha na machungu. Kumbe usilolijua ni kama usiku wa kaniki la kiza.

"Simama na tuende nyumbani. Heri nyumbani kuliko kupotelea mijini. Miji haitambui mja hasa wasichana wachanga mfano wetu. Salia papa hapa kijijini ipo siku.Mwalimu huyo alikuwa mwiba mkubwa sana katika jamii. Hebu fikiria aliyonitendea. Afadhali wewe alikataa kukulipia karo kwa sababu mama yako alikataa kutimiza matakwa yake ya kuolewa naye.

Wewe unadhani dunia imepasuka mahali? La hasha pengine kwa mfano wako na ami yako ni kweli kuna ufa duni unaopaswa kuzibwa kabla ya ukuta kuporomoka. Hata hivyo, kwa mujibu wa maelezo yangu sisi wasichana mara nyingi tunafanya maamuzi ambayo yanaweza kutumaliza na jamii zetu zote. Kukubali kuhusiana na mwalimu wangu amini usiamini kumeninyima baba na mama yangu. Nami nilikuwa nimejiunga na babu yangu. Sijui namna madaktari walivyonifufua. Kamwe usilie hupaswi kulia. Kunao wanaopaswa kulia. Kulia kwako ni mzaha mkubwa sana. Nani angefikiria kuwa siku moja ningerudi shuleni. Niwe miongoni mwa watahiniwa bora. Kumbuka Stadi asipochunga nitaongoza katika mtihani wa kitaifa. Ninaamini bidii zangu za mchwa ajengaye kichuguu kwa mate. Hata nawe amka. Kuvunjika kwa mwiko si mwisho wa upishi. Kumbuka pia kuteleza si kuanguka. Jizoe uanze safari tena. Msafiri ni yule aliye bandarini. Siku moja nakuahidi kisa chako hiki unachotaka kupoteza kwa kulia kutakuwa funzo kwa **mahuluki**.

Maisha ni safari isiyokuwa na likizo wala mapumziko. Maisha ni safari baharini inayohitaji nahodha mmoja, manahodha wengi chombo huenda mrama. Maisha ni uwanja wenye vituko na vitushi. Maisha ni sarakasi isiyokamilika. Usijute ungali hai. Licha ya hali yangu kiafya nimeamua kuandaa mustakabali mpya. Kamwe sitakuwa na athari yoyote hasi kwa maisha ya mtu. Nimeamua kujitenga na masuala ya mapenzi hadi pale nitakapoolewa na aliye na hali kama yangu.

Kumbuka siko peke yangu. Tuko wengi kama mchanga ufuoni. Usidhani kuwa u katika hali hiyo peke yako."

Maneno ya mwandani wangu yalinizindua nikazinduka. Yalizalisha tumaini moyoni mwangu. Yalinitia moyo na kunipa msukumo wa kuenda mbele. Nimeyasahau yaliyopita. Yakini, yaliyopita si ndwele tugange yajayo. Niliamua kamwe singetoka nyumbani mwetu kuenda mjini. Nilimsubiri mama kuja ili nimwarifu mabadiliko. Sitakata tamaa maishani. Nitaungana na sahibu yangu kusoma kwa bidii hadi tutakapokuwa wakili mashuhuri nchini. Lengo letu likawa ni kuwatetea wanyonge wanaonyongwa. Ipo siku itatimia. Hata tukiwa wakongwe waliokongeka na meno kung'oka.

Wiki mbili baadaye, nilipata ufadhili wa masomo yangu kutoka kwenye kundi la Linda Elimu Isipotee. Niliweza kuhamishwa na kupelekwa kwenye shule ya bweni. Ama kweli mnyonge ana sudi.

***Mwisho***

## MASWALI

1) Msimulizi alikuwa akiishi katika mazingira gani?
2) Eleza sababu zilizomfanya mwandishi kukata tamaa na maisha yake.
3) Jambo lipi lilikomfanya mwandishi kususia safari yake ya kwenda mjini kusaka ajira.
4) Kwa nini wanafunzi wengine walifurahi walipokuwa garini kwenda nyumbani baada ya kutumwa karo?
5) Hadaa alikuwa akiishi vipi alipokuwa katika uhusiano na mwalimu mkuu.
6) Eleza sifa za mwalimu mkuu.
7) Nani aliyekuwa akivisahihisha vijikaratasi vya Hadaa?
8) Eleza methali zozote utakozozitumia kumuonya Hadaa kama ungekuwa rafiki yake.
9) Matokeo yepi yaliyotolewa kwenye lebu?
10) Mbona Mwalimu mkuu hakuchukuliwa sheria baada ya unyama aliofanyia Hadaa?
11) Kwa nini daktari aliyemfanyia Hadaa vipimo alipewa uhamisho wa ghafla?
12) Je, mbona mamake Hadaa alibadili nia ya kutupilia mbali kesi dhidi ya mwakimu mkuu?
13) Mwandikie chifu wako barua ukimshauri dhidi ya umuhimu wa kulinda haki za watoto wa kike.

## MANENO MAPYA.

- ✓ **Kuuma meno** - kuvumilia.
- ✓ **Qurdusi** - jina la Mungu. Pia huitwa Mola , Rabana.
- ✓ **Mkata** - maakini. Mtu asiye na uwezo fulani.
- ✓ **Wandani** - marafiki.
- ✓ **Sudi** - kuwa na bahati.
- ✓ **Uhawinde** - ufukara.
- ✓ **Kishirazi**- kingulima cha mchwa pia huitwa Kichuguu.
- ✓ **Ami** - ndugu wa kiume wa baba.
- ✓ **Hawafu** - uoga au wasiwasi.
- ✓ **Hisiamseto**- kuwa na mchanganyiko wa mawazo ya hofu
- ✓ **Subu** - shambulia, tusi au tukana mtu.
- ✓ **Kunigoga**- kushtua.
- ✓ **Bilula** - koki.
- ✓ **Dhikiri** - hali ya kukumbuka wema wa Mola. Pia huitwa dhukuru.
- ✓ **Siwa** - aina ya paragumu kubwa.
- ✓ **Sikumaizi** - sikujua.
- ✓ **Chuchunge** - samaki
- ✓ **Mbawazi**- huruma
- ✓ **Hiari**- kufanya kitu bila kushurutishwa na mtu.
- ✓ **Rangaito** - hofu, wasiwasi.
- ✓ **Belele**- tele
- ✓ **Chudere** - kichinjamimba.
- ✓ Hamamuni - sehemu ya kuogea. Pia huitwa bafu.
- ✓ **Maninga**- macho

- ✓ **Sadaruki** - chumba cha wagonjwa mahututi.
- ✓ **Tete**- takataka zinazoungua motoni
- ✓ **Kidigi**- uchache wa kitu. Pia huitwa kidinya au kiduchu.
- ✓ **Mahukuki** - watu.